Ghadhabu Ya Mungu

na

Ellis P. Forsman

Ghadhabu Ya Mungu

na

Ellis P. Forsman

Octoba 15, 2011

Ghadhabu Ya Mungu

Rum. 1:18-32

Andiko linazungumzia siku inayokuja ya ghadhabu ya Mungu…

Ikifunua hukumu ya haki ya Mungu.

Rum. 2:4-6, "*Au waudharau wingi na wema wake na ustahimilivu wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu? Bali kwa kadiri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea hakiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.*"

Siku ya hukumu kwa wasiyomcha Mungu.

2 Pet. 3:7, "*Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto kwa neon lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, nay a kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.*"

Ambapo haki ya Mungu iliyokamilika hujulikana. Maandiko pia huzungumzia jinsi ghadhabu ya Mungu ilivyokwisha kuja…

Imefunuliwa kutoka mbinguni.

Rum. 1:18, "*Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni na uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu.*"

Dhidi ya wote wasio na Uungu na wanadamu wote wasio haki.

Ambayo walioonja haki ya Mungu ufunuliwa.

Kwa nini Mungu huonyesha ghadhabu yake? Anaonyeshaje ukarimu wa haki yake hata leo, muda mrefu kabla ya Siku ya Hukumu? Kifungu chetu (Rum. 1:18-32) inatoa majibu.

Kwa nini Mungu anadhihirisha dhadhabu yake

Kwa sababu mwanadamu hufanya ugumughadhabu ya Mungu iliyodhihirishwa…

Kwa kuonyesha ghadhabu kwa wasiohaki.

Rum. 1:18, "*Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni na uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu.*"

Kwa kukataa iliyo kweli. Wakipinga kilicho cha uungu na haki.

Kwa kupindisha ambacho Mungu tayari amekidhihirisha.

Rum. 1:19-20, "*Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani uweza wake wa Uungu wake hata wasiwe na udhuru;*"

Vitu vya Mungu vinavyodhihirishwa kwa mwanadamu mwenyewe huonyesha uwepo wa Mungu.

- Kama vile, uwezo wa mwanadamu na utu wake, hunyesha sawa na Muumba wake.
- Kama vile, hisia ya mwanadamu la kusudi, ikionyesha Muumbaji mwenye haki.

Vitu vya Mungu vinavyodhihirishwa katika uumbaji unaomzunguka kuthibitisha uwepo wake.

Zab. 19:1-2, "*Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake. Mchana husemezana na mchana, usiku hutolea usiku maarifa.*"

Sifa zisizooneka za Mungu, huonekana na kueleweka kwa vitu vinavyoonekana. Kama vile, mtindo na mfumo wa anga uonyesha uwezo wa umilele na ukuu.

Mwanadamu anaposhindwa kusikiliza uzuri na mfumo wa anga ambao hutangaza "uwepo wa Mungu!", Mungu amechukia!

Kwa sababu mwanadamu hanashukurani na mjinga

Kutokuwa na shukurani kwa Mungu.

Rum. 1:21, "*Kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu <u>wala kumshukuru</u>; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza.*"

Hata walipomfahamu; bado walishindwa kumtukuza kama ndiye Mungu.

Wakawa wazushi na wajinga katika mioyo yao.

Rum. 1:21-23, "*Kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru, bali <u>walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza.</u> Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya kibinadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo.*"

Madhara ya kutomtukuza Mungu.

Upelekea katika uasherati (kuabudu kiumbe kuliko Muumba).

- Wanamfanya Mungu kwa mfano wao.
- Wakimfanya Mungu kwa mfano wa viumbe vingine.

Mwanadamu wa kisasa ana mungu wake.

- Kama vile, kuabudu nafsi.
- Kama vile, tama (kuabudu pesa au vitu).
- Efe. 5:5, "*Maana neon hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tama, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu.*"
- Kol. 3:5, "*Basi vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tama mbaya, mawazo mabaya, na kutamani ndiyo ibada ya sanamu.*"

Mwanadamu anapoaacha kumshukuru Mungu, na kuviinua vilivyoumbwa juu ya Mungu, basi Mungu anachukia!

Ghadhabu ya Mungu siku ya mwisho itahusisha mwisho wa kutisha.

- 2 Pet. 3:10, "*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.*"
- 2 Thes. 1:7-9, "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto, huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoangamizwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake.*"

Ghadhabu ya Mungu inapofunuliwa leo inatisha, lakini pia ni hatari.

Jinsi Mungu anavyoonyesha ghadhabu Yake

"Anamtoa mwanadamu" katika uchafu

Mungu *"aliwaachilia".*

Rum.1:24, "*Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tama za mioyo yao, waufuate uchafu, hata wakavunjiana heshima miili yao.*"

Hakuna moto utokao mbinguni kuwachoma; bali umwacha mwanadamu katika tama zake.

Hakuna uchafu.

Katika tama ya mioyo yao (popote ambapo mioyo yao iliyo miovu uwaongoza).

Marko 7:21-23, "*Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivu, uuaji, uzinzi, tama mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi.*"

Kwa nini Mungu anawaachilia? Kwa sababu wamebadilisha ukweli wa Mungu kuwa uongo.

Rum. 1:25, "*Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina.*"

Kukiabudu na kutumikia kile kilichoabudiwa.

Badala ya yeye aliyeumba na anafaa kutukuzwa milele.

"Amamwacha mwanadamu" katika tama mbaya

Tena Mungu "*aliwaachilia*".

Rum. 1:26-27, "*Hivyo mungu aliwaacha wafuate tama zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili; wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke ya asili, wakawakiana tama wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao.*"

Hakuna radi utokao mbinguni kumpiga mtu, bali umwacha mtu katika tama zake mbaya.

Katika swala hili, kufanya tendo la ndoa na wanyama pamoja na usodoma. Wanawake kubadilisha matumizi ya asili kwa kile ambacho siyo asili. Wakitumia miili yao kwa wanawake wengine badala ya njia ambayo Mungu alikusudia. Na wanaume wakiacha matumizi ya asili ya wanawake. Wakitumia miili yao kwa wanaume wengine badala ya njia ambayo Mungu alikusudia.

"*Wakipokea thawabu ya udhalimu wao ambayo ilimanishwa.*" (wakipata madhara ya upotevu wao ambaoyo iliisha (kama vile AIDS)

"Anamwachilia mwanadamu" katika akili iliyovurugika na kutokuwa na haki

Tena Mungu "*aliwatoa*".

Rum. 1:28, "*Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wayafanye yasiyowapasa.*"

Kwa kuwa hawakutaka kuwa na Mungu katika akili zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wafanye mambo yasiyowapasa.

Matokeo ya "kuachwa": kujazwa na visivyo haki.

Rum. 1:29-31, "*Wamejawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tama na ubaya, wamejawa na husuda na uuaji, na fitina na hadaa, watu wa nia mbaya wenye kusengenya, wenye kusingizia wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasiotii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema;*"

Wanafahamu hukumu ya Mungu ya haki, kwamba watu kama hao wanafaa kufa.

Rum. 1:32, "*Ambao wakijua sana hukumu ya haki ya Mungu, ya kwamba wayatendao hayo wamestahili mauti, wanatenda hayo wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nayo wayatendao.*"

Bado wanayafanya. Alafu wanawashutumu wale wanaoyafanya.

Hitimisho

Ghadhabu ya Mungu huonyeshwa leo kwa kumruhusu tu mwanadamu kwenda katika njia yake…

- Kufuata tamaa ya moyo wake.
- Kufuata mvuto wa tama zake.
- Kujikwaa katika ukengeufu wa upofu ili kuongeza upotevu.

Efe. 4:17-19, "*Basi nasema neon hili tena nashuhudia katika Bwana, tangu sasa msienende kama mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao; ambao akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani.*"

Huruma ya Mungu hudhihirika leo kwa wale wanaopenda kumgeukia

Wakipenda kutangaza ufunuo wake...

Uliyotolewa kupitia uumbaji

Na zaidi sana ikitolewa kupitia Mwanawake!

1 Yoh. 4:9-10, "*Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma mwanaye pekee ulimwenguni ili tupate uzima kwa yeye. Hili ndilo pendo si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba alitupenda sisi, akamtuma mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu.*"

Wakiwa tayari kushukuru...

Wakiwa na tabia ya shukurani.

- Kol. 1:12, "*Mkimshukuru Baba aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru.*"
- Kol. 2:7, "*Wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa mkizidi kutoa shukrani.*"
- Kol. 3:15, "*Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu, ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja, tena iweni watu wa shukrani.*"
- Kol. 3:17, "*Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*"
- Kol. 4:2, "*Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani;*"

Tukionyesha shukrani kupitia toba.

Rum. 2:4, "*Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimilivu wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu?*"

Je sisi ni watu wa shukrani? Tunaionyesha kwa kugeuka kutoka katika dhambi zetu na kumgeukia Mungu? Kama siyo, tuna kila sababu ya kuogopa ghadhabu ya Mungu – siyo tu Siku ya Hukumu, bali madhara katika maisha haya ya Mungu "*kutuachilia*" katika tama zetu!